ILANI YA UCHAGUZI YA WANAWAKE

UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2019 NA UCHAGUZI MKUU 2020

Ajenda ya Mwanamke, Turufu ya Ushindi 2019/2020

TGNP Mtandao

MTANDAO WA WANAWAKE NA KATIBA

WOMEN FUND TANZANIA
Empowering Local Women Heroes

ILANI YA UCHAGUZI YA WANAWAKE

UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA 2019 NA UCHAGUZI MKUU 2020

Ajenda ya Mwanamke, Turufu ya Ushindi 2019/2020

UTANGULIZI

Ilani hii inaendeleza madai ya wanawake watetezi wa haki za ushiriki katika uongozi wa kisiasa tangu tupate uhuru hadi leo. Ilani hii ni ya tano iliyobeba madai yetu rasmi tukiwa wadau na washiriki wakuu katika michakato mbalimbali ya uchaguzi. Ilani ya kwanza ilikuwa ya mwaka 2000 ikijulikana kama Ilani ya Wapiga Kura, Ilani ya pili ni ya mwaka 2005, ya tatu ni ya mwaka 2010 na ya nne ni ya mwaka 2015. Maandalizi ya ilani zote nne yaliongozwa na TGNP Mtandao kwa kupitia Mtandao wa Wanawake na Katiba, Uchaguzi na Uongozi. Ilani hii ya tano inajumuisha sauti za Wanawake kutoka makundi mbalimbali chini ya uongozi wa TGNP Mtandao kwa kushirikiana na Women Fund Tanzania na Mtandao wa Wanawake na Katiba, Uchaguzi na Uongozi.

Sisi wanawake wapiga kura, tunatambua kwamba sisi ni wadau muhimu katika shughuli zote za kisiasa na maendeleo ya jamii zetu. Idadi yetu tukiwa wapiga kura, wanachama wa vyama vya siasa na tukiwa wazalishaji wanaoendeleza kizazi cha taifa ni kubwa na haiwezi kupuuzwa. Tunatambua na kudai haki za kushiriki katika uchaguzi kama wapiga kura na wanaowania nafasi za uongozi, walioteuliwa na kugombea hatimaye wenye kushinda nafasi mbalimbali za uongozi kwa kupitia uchaguzi. Haki hizi zimebainishwa katika mikataba mbalimbali ya kimataifa, kikanda na katika sheria, sera na katiba ya nchi.

Mikataba hii ni pamoja na Tamko la Kimataifa Kuhusu Haki za Binadamu (UDHR 1948) Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (CEDAW 1979, Kifungu cha 7: a, b na C), Mapendekezo ya baraza la Usalama (UNSC 1325 (2000). Mpango Kazi wa Beijing (1995), Malengo ya Milenia ya Maendeleo (Lengo la 3), pamoja na Mkataba wa Afrika Kuhusu Haki za Binadamu ikiwa ni pamoja na Mkataba wa Ziada wa Maputo. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) imebainisha haki za wanawake za kushiriki katika nafasi za maamuzi ikiwa ni pamoja na ushiriki wao katika uchaguzi wakiwa

wapiga kura na wagombea nafasi mbalimbali za uongozi. Vilevile, azma ya kutokomeza aina zote za ubaguzi wa kijinsia imebainishwa katika Dira ya Taifa ya mwaka 2025 inayokiri kwamba, ifikapao mwaka wa 2025, taifa letu litakuwa limetokomeza aina zote za ubaguzi wa kijinsia. Hivyo basi, sisi wanawake wapiga kura kwa mara nyingine tena tunaendelea kupaza sauti na kusema, tunadai kushiriki kikamilifu katika mchakato wote wa chaguzi za mwaka 2019 wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ili hatimaye tuweze kushiriki katika meza za maamuzi kikamilifu katika nyanja mbalimbali za Taifa.

Sisi ni nani?

Ilani hii ni jumuisho la sauti za pamoja za Wanamtandao wa Wanawake na Katiba, Uchaguzi na Uongozi waliotoka kwenye asasi za kiraia takribani 60 kutoka ngazi za kijamii na Kitaifa. Mtandao wa Wanawake na Katiba, Uchaguzi na Uongozi ulianza rasmi wakati wa mchakato wa kuandaa Katiba mpya na kuendelezwa wakati wa uchaguzi wa mwaka 2015 hadi leo hii. Lengo kuu la Ilani hii ni kudai ushiriki wetu katika uongozi wa Taifa letu ikiwa ni pamoja na ushiriki katika chaguzi zote kama wapiga kura, waliotueliwa kuwania nafasi mbalimbali katika uchaguzi, washindi na waliopewa dhamana ya kuongoza taifa letu katika nyadhifa mbalimbali kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Ilani hii inamlenga nani?

Awali ya yote, Ilani hii inatuhamasisha sisi Wanawake, wapiga kura tukatae kuendelea kutumiwa kama wapiga debe, wasindikizaji katika kampeni, waburudishaji kwenye sherehe au kampeni za uchaguzi na wahanga wa ufukara na umaskini. Tuhamasike na kushikamana ili kupambana na mifumo kandamizi hususani mfumo dume, ambayo huathiri upatikanaji wa haki zetu na hatimaye kudumaza uchumi na maendeleo ya jamii yote, wake kwa waume.

Vile vile Ilani inalenga vyama vya siasa, tangu wanachama, uongozi na mashabiki wa vyama hivyo. Hapa kwetu Tanzania, vyama vya siasa ni njia pekee ya kuingia kwenye kinyang'anyiro cha uchaguzi. Hivyo basi vyama vya Siasa ni walinzi wa Lango kuu la kuingia kwenye siasa za uchaguzi. Kwa maana hii vyama vya Siasa ndivyo huamua ni nani aingie na ni nani aachwe, ni nani awezeshwe kushinda na pia ni nani aachwe akiogolea mwenyewe kwenye uwanja wa ushindani usiyo haki na huru kwa wanawake walio wengi.

Tatu, Ilani hii inalenga serikali kuu iliyoko madarakani na ile itakayoshika madaraka na taasisi zake. Serikali iliyoko madarakani ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kuwa uwanja wa ushindani wa kisiasa ni huru na wa salama kwa makundi yote hususani wanawake. Serikali tutakayoipa dhamana ya kutuongoza kwa kipindi kingine cha miaka mitano ituhakikishie ushiriki wetu katika nyanja zote za uongozi.

Vilevile, Ilani inalenga vyombo vya habari kutokana na uwezo wao wa kugusa mtazamo wa jamii kuhusu nafasi ya wanawake katika uongozi na maendeleo ya taifa letu.

Mwisho, Ilani inalenga wapiga kura wote wanawake kwa wanaume, vijana kwa wazee. Kwa Wapiga kura wanawake, tunatoa wito kwao kutambua kwamba kura zao ni Turufu ya Ushindi kwa Vyama vyao vya Siasa na Wagombea!!

MUKTADHA

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 na Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ni wa kihistoria kwenye harakati za ukombozi wa wanawake kimapinduzi hapa nchini Tanzania. Mwaka huu wa 2019 kuelekea mwaka 2020 tunasherekea kuzaliwa kwa Asasi nyingi za kupigania haki za wanawake hapa nchini ikiwa ni pamoja na Taasisi ya Mtandao wa Jinsia Tanzanaia (TGNP Mtandao). Wakati huo huo mwaka huu tunajiandaa kusherekea kuelekea mwaka 2020, miaka 25 ya Mpango Kazi wa Bejing ulobainisha maeneo 12 ya kipaumbele ikiwa ni pamoja na ushiriki wa wanawake katika ngazi zote za maamuzi. Tunapojiandaa kwa chaguzi hizi mbili muhimu, Wanamtandao, watetezi wa haki za wanawake, tunatafakari tulikotoka, mafanikio yetu, changamoto tulizokabilina nazo, na mikakati ya kukabiliana na changamoto hizo. Hivyo basi, kipindi hiki ni kipindi muhimu kitakachowezesha kutafakari kuhusu maendeleo yetu kwa ujumla wakati huo huo kikiwa ni kipindi cha kubainisha mbinu mbadala za kuendeleza mapambano yetu ya kuongeza Wanawake katika uongozi wa kisiasa.

Hali ya ushiriki wa wanawake na uchumi nchini (“Uchumi Umekua lakini pengo la Jinsia ni kubwa”)

- Kwa kipindi cha mwongo mmoja pato la taifa limeongezeka kwa kasi ya asilimia 6-7
- Sekta zilizokua ni zile ambazo hazigusi maisha ya mwanamke hususani wa kijijini moja kwa moja, ikiwa ni pamoja na sekta ya fedha, ujenzi, mawasiliano na utawala wa umma.
- Asilimia 65 ya wakulima wadogo wadogo ni wanawake, lakini sekta hii haikui kwa kasi kama sekta nyingine.
- Wanawake walio wengi hawamiliki ardhi, na mashamba wanayomiliki ni madogo zaidi kuliko ya wanaume kwa kiasi cha asilimia 40.
- Asilimia 70 ya chakula kinacholisha kaya kinatokana na nguvu kazi ya wanawake.

- Umaskini uliokithiri unabeba sura ya kijiji na ya mwanamke.
- Ubadhirifu na rushwa ikiwa ni pamoja na rushwa ya ngono vinachangia kwenye kudhoofisha jitihada na azma ya kuwezesha kukua kwa uchumi linganifu na mpana.
- Wanawake wako zaidi kwenye ajira zenye ujira mdogo na wengi wako kwenye sekta isiyo rasmi.
- Kwenye sekta ya ajira rasmi, mishahara ya wanawake ni midogo kuliko ya wanaume(URT (NBS: 2018)

Ustawi wa Jamii na Usawa wa Jinsia

"Ujinga, maradhi na umaskini" vilibainishwa na hayati Mwl Julius Nyerere (Muasisi na Raisi wa Kwanza Tanzania) kama maadui watatu waliokabili Taifa la Tanzania wakati tulipopata uhuru.

Umaskini na Ubora wa Maisha

Takwimu rasmi zinaonesha kuongezeka kwa ubora wa hali ya maisha (URT & UNDP 2015) lakini kuna mapengo ya jinsia na ya kitabaka katika hali ya ubora wa maisha hapa nchini.

- Umaskini kwa jumla ulipungua kutoka asilimia 64 mwaka 2010 hadi asilimia 47 mwaka 2015
- Umaskini uliyokithiri ulipungua kutoka asilimia 31.3 mwaka 2010 hadi kufikia asilimia 17.7 mwaka 2015.
- Hata hivyo, mwanamke wa Tanzania hususan wa vijijini ameendelea kubeba mzigo wa ziada utokanao na athari za umaskini na ubaguzi wa jinsia.

Elimu: Ufikiaji Elimu kwa Wote na Haki ya Mtoto wa Kike

- Kumekuweko na usawa wa jinsia katika ufikiaji wa elimu ya awali, ya msingi na hata sekondari hadi kidato cha nne.

- Idadi au kiwango cha kumaliza elimu ya ngazi tajwa ni kubwa kwa wasichana kuliko hata wavulana.
- Hata hivyo uwiano huu unabadilika katika ngazi ya kidato cha tano na sita, ambapo wavulana wengi zaidi huingia na hatimaye kuingia vyuo vikuu kwa asilimia kubwa zaidi kuliko wasichana.

Afya na haki za wanawake

- Jitihada za kuongeza ubora na ufikiaji wa huduma za afya kwa watanzania walio wengi zimeendelea kuwepo
- Changamoto kubwa ni vifo vya wanawake kutokana na uzazi havijapungua kwa kiwango cha kuridhisha. Takriban wanawake 556 kati ya kila vizazi hai 100,000 wanapoteza maisha wakati wanapozalisha nguvu kazi ya taifa hili (TDHS, 2015-2016).
- Vifo vya uzazi vinatokana na mambo yanayoweza kuzuilika endapo uhai na mchango wa wanawake katika Taifa utapewa kipaumbele kwenye mipango mikubwa ya Taifa.

Ukatili wa Jinsia

Kwa kutambua kuwepo na kushamiri kwa ukatili wa jinsia na athari zake kubwa kwa wanawake na watoto wa kike, Serikali ya Tanzania imetayarisha Mpango wa Kuzuia na Kutokomeza Ukatili wa Jinsia: 2017/18-2021/22. Takwimu zinaonesha hali ya ukatili wa jinsia kama ifuatavyo:

- Asilimia 45 ya wanawake kati ya umri wa miaka 15-49 wamekuwa wahanga wa ukatili wa jinsia nchini. Asilimia 25 ikiwa ni ukatili wa kuumiza mwili, asilimia 7 ukatili wa kingono na asilimia 14 ukatili wa kuumizwa kimwili na kingono
- Asilimia 60 ya wanawake wameumizwa kisaikolojia na vitendo vya ukandamizaji dhidi yao.
- Asilimia 27 ya watoto wa kike wenye umri kati ya 15-19 aidha ni wajawazito au wana watoto. (NBS 2016 na 2018)

Ushiriki wa Wanawake katika Uongozi

Ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi (hasa ya kisiasa) bado ni mdogo, hali ambayo inakinzana na azma ya kujenga jamii isiyokuwa na ubaguzi kama ilivyobainishwa kwenye dira ya Taifa 2025, Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, pamoja na sheria mbalimbali za nchi.

Hali ya Ushiriki wa Wanawake (kipindi cha awamu ya tano)

- Katika ngazi zote za uongozi wanawake ni asilimia ndogo.
- Uchaguzi wa mwaka 2015 ulivunja rekodi ya kumchagua Makamu wa kwanza wa Rais mwanamke tangu tupate uhuru
- Uwaziri ni asilimia 17.
- Makatibu Wakuu ni asilimia 11 tu.
- Wakuu wa Mikoani asilimia 23 (kulinganisha na asilimia 28.5 kipindi cha 2010/2015)
- Wakuu wa wilaya ni asilimia 28 (kutoka asilimia 35.3 katika kipindi cha 2010/2015) (NEC:2016)

Ushiriki wa Wanawake Katika Siasa na Uchaguzi

Ngazi ya Ubunge:

Wanawake wanaoteuliwa na vyama vya siasa kuwania nafasi ya ubunge wa kuwakilisha jimbo ni ndogo, na hatimaye wanaoshinda ni kidogo zaidi. Wanawake wachache sana huteuliwa na vyama vyao kuwania nafasi za uchaguzi. Kwa mfano:

Katika uchaguzi wa mwaka 2015, vyama viliteua wagombea wanawake kama ifuatavyo:-

CCM

Asilimia **9**

CHADEMA

Asilimia **6**

CUF

Asilimia **11**

ACT Wazalendo

Asilimia **15**

Vilivyobaki vilichukuliwa na vyama vingine.

- Katika uchaguzi wa mwaka 2015, kulikuwepo na wagombea wa viti vya ubunge 1,250 kwa Tanzania Bara. Kati yao, wanawake walikuwa 238(19%) tu.

- Katika ngazi ya udiwani, kati ya wagombea 10,879, wanawake walikuwa 679 (6.2%) tu. (CEMOT:2016, TGNP 2015), ripoti ya wachunguzi wa uchaguzi (CEMOT) inatahadharisha kwamba hatua za makusudi zisipochukuliwa kurekebisha hali hii, itachukua chaguzi 31 au miaka 155 kurekebisha hili pengo la jinsia.

Kurekebisha uwiano sawia wa uwakilishi katika ngazi hii, serikali ilichukua hatua za makusudi za kikatiba kwa kuwepo kwa viti Maalum.

- Viti Maalum vimewezesha ongezeko la wanawake katika vyombo vya uwakilishi. Kwa mfano katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge la 9 lilikuwa na wawakilishi wanawake kupitia viti maalum 75 au asilimia 74.2 ya Wabunge wanawake. Idadi hii na kiwango kiliongezeka kufikia 102 au asilimia 78.5 ya wabunge wote

wanawake. Katika Bunge la 11 idadi iliongezeka kidogo na kufikia 113 au asilimia au asilimia 79.3 kati ya Wabunge Wanawake 145. (NEC, miaka husika)

Pamoja na kwamba viti maalum vimewezesha kuongezeka kwa uwakilishi na sauti za wanawake katika muhimili huu mkuu wa utawala, utekelezwaji wake umekuwa na changamoto.

Wawakilishi wanaopitia viti maalum hubaguliwa katika kushika baadhi ya nyadhifa kama vile Waziri Mkuu, hubaguliwa katika kupewa fedha za majimbo, na kwenye baadhi ya vyama vya siasa hakuna uwazi kwenye uteuzi wao.

Uongozi wa Vyama vya Siasa.

Azma ya kuanzishwa kwa siasa ya Vyama vingi ni kujenga demokrasia shirikishi inayoongozwa na misingi ya usawa, utawala bora na kuheshimu haki za binadamu. Hata hivyo kuanzishwa kwa vyama vingi hakujaleta mabadiliko makubwa kwenye usawa wa jinsia, heshima ya haki za wanawake na makundi yaliyoko pembezoni, wala ushiriki wa wanawake na makundi ya pembezoni kwenye uongozi wa Vyama. Kwa mfano:

- Tangu kuanzishwa kwa vyama vingi, nafasi ya wenye viti wa vyama imehodhiwa na wanaume, isipokuwa chama kimoja kilichomchagua mwanamke kama Mwenyekiti ambaye hakuwa msemaji wa mwisho wa Chama husika.
- Kuna vyama 3 (16%) tu vyenye wanawake walioshika wadhifa wa Ukatibu Mkuu wa Vyama vyao kati ya vyama 19. Na kati ya Manaibu wasaidizi 38 wa vyama vya siasa, kuna wanawake 4 tu sawa na asilimia 14 ya Manaibu Katibu wakuu wa Vyama
- Wanawake ni wachache kwenye nyadhifa za ukurugenzi na shughuli nyingine zinazohitaji uongozi. Hata hivyo vyama vyote vinategemea sana nguvu kazi ya wanawake katika kuhamasisha wanachama, katika kutafuta rasilimali fedha na katika kampeni za vyama wakati wa uchaguzi.

Kwa ufupi ushiriki wa wanawake katika nyanja mbalimbali za kisiasa umekuwa finyu kama tulivyoonesha. Kwa kuzingatia ufinyu huo, sisi Wanamtandao wa Wanawake na Katiba, Uchaguzi na Uongozi, kwa sauti moja tunapaza sauti zetu tukibainisha madai yetu kwa wadau wahusika kwenye zoezi lote la uchaguzi.

MADAI YA WANAMTANDAO WA WANAWAKE NA KATIBA NA UCHAGUZI

Madai kwa Serikali iliyoko Madarakani

Sisi Wanawake wapiga kura, tunatambua kwamba serikali iliyoko madarakani pamoja na vyombo vyote vya dola na taasisi zake zote ina jukumu na wajibu wa:

- Kuweka mazingira wezeshi na salama kwa wanawake na watu wenye changamoto za kimaumbile wakati wote wa zoezi la uchaguzi.
- Kuhakikisha wadau wote wa uchaguzi wanazingatia misingi ya ushindani wa haki na huru na usawa wa jinsia kama ilivyoainishwa kwenye Katiba, sheria, sera, mipango ya nchi na kubainishwa kwenye mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo serikali yetu imeridhia.
- Kuhakikisha na kusimamia vyombo vyote vya dola vilivyopewa dhamana ya kusimamia uchaguzi vinazingatia miongozo, na sheria zenye kulinda wanawake dhidi ya matendo ya udhalilishwaji wakati wa uchaguzi.
- Kusimamia uzingatiaji wa misingi ya usawa wakati wa uteuzi wa wagombea wanawake ndani ya vyama,
- Kusimamia matumizi ya rasilimali fedha hususani ruzuku zitokanazo na kodi ya Watanzania ili kuhakikisha zinatumika kwa madhumuni ya kuziba mapengo ya jinsia wakati wa uchaguzi.
- Kusimamia vyombo vya habari wakati wa uchaguzi ili vitoe fursa sawa kwa wagombea wote wakati wote wa kampeni. Pamoja na kuhakikisha kwamba vyombo vya habari havitumiki kuendeleza utamaduni wa kumdhalilisha mwanamke hususani wale wanaowania nafasi ya uongozi wakati wa uchaguzi.

- Kuhakikisha na kusimamia vyombo vyote vya dola na taasisi zake vilivyopewa dhamana ya kusimamia uchaguzi, utawala bora, na demokrasia shirikishi kwa mrengo wa jinsia. Vyombo hivi ni pamoja na:

- **Tume ya Taifa ya Uchaguzi**- Kuhakikisha na kuwajibisha Tume isimamie misingi ya haki, usawa, utawala bora katika kuteua wasimamizi wa uchaguzi, kubainisha mipaka na majimbo ya uchaguzi kusimamia elimu ya uraia yenye kuzingatia misingi ya usawa wa jinsia na demokrasia shirikishi, kusimamia zoezi lote la uchaguzi tangu kabla ya uchaguzi, wakati wa kupiga kura na hatimaye baada ya kupiga kura. Kutoa ripoti yenye kuonesha mafanikio, changamoto na mafunzo ikibainisha masuala ya jinsia wakati wa mchakato wote.

- **Msajili wa Vyama vya Siasa**- Kuhakikisha Msajili wa Vyama vya Siasa anatoa miongozo kwa Vyama vya Siasa yenye tafsiri ya kuongoza Vyama kuzingatia haki za wanawake na watu wenye ulemavu kwenye kushiriki katika uongozi wa Vyama vyao kama ilivyoainishwa kwenye katiba ya Nchi, mikataba ya kimataifa na kanda pamoja na Sheria ya Vyama vya Siasa-2019 (kifungu 6A). Kusimamia na kutoa elimu ya uraia na mpiga kura inayoingiza elimu kuhusu haki za wanawake na watu wenye ulemavu katika uongozi na uchaguzi.

- **TAKUKURU**- Kudhibiti na kupambana na Rushwa ikiwemo Rushwa ya Ngono kama ilivyobainishwa kwenye kifungu cha 25 cha sheria namba 11 ya mwaka 2007 ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa wakati wa uchaguzi.

- **Jeshi la Polisi**- litambue kuwa jukumu lao kubwa ni ulinzi wa raia wote, wake kwa waume. Jeshi hili liepukane na tabia ya kutumia nguvu wakati wa uchaguzi kwa raia wasio na makosa, na pale penye ukiukwaji wa sheria au taratibu, kutumike busara ya kuelimisha au kuchukua hatua stahiki.

- **Mahakama**- kushuguhulikia kesi za Uchaguzi kwa kutumia hekima ambao haiendelezi ukiukwaji wa haki za wanawake na watu wenye ulemavu.

- **Tume ya Haki za Binadamu**- Kusimamia uzingatiaji wa haki za wanawake na watu wenye ulemavu kwenye mchakato mzima wa uchaguzi

3.2 Madai kwa Vyama vya Siasa

Sisi Wanawake na wapiga kura, tunatambua kwamba Vyama vya Siasa ni mhimili mkubwa kwenye kujenga jamii inayozingatia demokrasia shirikishi na yenye mrengo wa jinsia. Vilevile, Vyama vya Siasa hapa kwetu Tanzania, ni walinzi wakuu kwenye lango la kuingia kwenye kinyang'anyiro cha siasa. Vyama vina uamuzi wa mwisho, wa ni nani aingie na ni nani aachwe nyuma. Hivyo basi vyama vya siasa vina wajibu wa kuweka misingi na mfumo wezeshi wa ushiriki kamilifu wa wanawake na watu wenye ulemavu katika uongozi ndani ya vyama na nje ya vyama kwa kufanya yafuatayo:

- Vichukue hatua za makusudi za kuziba mapengo ya jinsia ndani ya uongozi wa Vyama
- Vijiwekee kanuni zinazowajibisha viongozi wa Vyama kutokunyanyasa wanawake aidha ndani ya Vyama au nje ya Vyama
- Katika uteuzi wa wagombea wote wa nafasi za ushiriki, wanawake wasipungue asilimia 50 kama ilivyoainishwa kwenye Mkataba wa Maputo
- Kuwa na utaratibu wa kusimamia matumizi ya fedha hususani fedha za ruzuku kutoka serikalini zitumike kwa njia ya kupunguza mapengo ya jinsia ndani ya uongozi wa vyama na wakati wa uchaguzi wa Kitaifa
- Vyama viweke mikakati ya kuwezesha wanawake na makundi maalum katika kampeni ili washinde
- Viendeshe siasa kwa kutumia nguvu za hoja na siyo nguvu za misuli

- Viwe na ajenda za kushawishi kuingiza masuala ya jinsia kwenye ajenda kuu ya Vyama vyao
- Vihamasishe wanachama wao kutambua faida ya kuzingatia misingi ya usawa, hususani kushirikisha wanawake katika nafasi za maamuzi katika vyama vyao.

Madai kwa Wagombea Uongozi

Siasa iliyojikita kwenye misingi ya ushindani wa haki, huru na uwazi inawezekana tu pale ambapo wagombea wote wanaonesha utayari wa kushinda au kushindwa kwa kutumia ushawishi, nguvu za hoja na kuheshimu wagombea wengine. Hivyo basi, sisi Wanawake wa Mtandao wa Katiba, Uchaguzi na Uongozi tunatoa rai kwa wagombea wote kutambua wajibu wao kwenye kutekeleza azma ya uchaguzi ulio wa haki, huru na salama kwa wagombea wote na wapiga kura wote. Hivyo basi, wagombea wote wanapaswa kuwajibika kwa kufanya mambo yafuatayo:

- Ajielimishe taratibu zote za uchaguzi ikiwa ni pamoja na miongozo na sheria zinazoelekeza uzingatiaji wa haki za wagombea wa kike na wa kiume
- Aendeshe kampeni zilizo salama kwa wanawake wapiga kura na wanachama chake
- Awe na ajenda yenye kubeba ajenda ya ukombozi wa mwanamke kimapinduzi
- Aoneshe kwa vitendo imani yake kwenye kuheshimu haki za binadamu hususani, wanawake na watu wenye ulemavu
- Aepuke matumizi ya lugha yenye kudhalilisha wanawake na watu wenye ulemavu
- Aepuke na kukemea vitendo vya rushwa ikiwemo rushwa ya ngono

Madai kwa Vyombo vya Habari

Sisi Wanawake wapiga kura na wadau wa habari, tunatambua kwamba Vyombo vya habari ni mhimili muhimu wenye uwezo wa kuleta mabadiliko makubwa kuhusu mtazamo wa jamii kuhusu nafasi ya mwanamke katika uongozi. Vyombo vya habari vina uwezo mkubwa wa kuathiri matokeo ya uchaguzi na kuathiri matokeo ya ushindi au kushindwa kwa wanawake kwenye uchaguzi. Kwa mantiki hii, vyombo vya habari vina wajibu wa kufanya mambo yafuatayo:

- Kuelimisha jamii kuhusu haki za wanawake
- Kutoa fursa kwa wagombea wanawake ili waweze kujinadi kwa wapiga kura kwa bei nafuu
- Kuepuka tabia ya kuwadhalilisha wanawake kwenye vyombo husika
- Kutoa kipaumbele kwenye kuhabarisha jamii kuhusu matukio yenye jumbe za utetezi wa wanawake

Madai kwa wapiga Kura, Wanawake kwa Wanaume

Ushindi wa wanawake kwenye uchaguzi utategemea sana uamuzi wa wapiga kura, wake kwa waume. Kwa kuzingatia kwamba wanawake ni asilimia kubwa zaidi ya wapiga kura wote, basi sisi wanawake wapiga kura tunatoa rai kwa wapiga kura wote, hususani wanawake kuwapigia kura, wanawake wenye uwezo na wenye kubeba ajenda ya ukombozi wa mwanamke kimapinduzi wanapojitokeza. Tunatoa rai kwa Wapiga kura wote kufanya mambo yafuatayo:

- Kuhamasisha wanawake wenye uwezo kujitokeza kwenye kuwania nafasi za uchaguzi, tuna uhakika wapo.
- Kushawishi Vyama kuteua wanawake wenye uwezo kuwania nafasi za uongozi, tuna uhakika wapo.
- Kuwapa moyo wale wanawake waliojitokeza kuwania viti vya uchaguzi

- Kuwapigia kura wanawake wenye uwezo bila kujali itikadi za vyama vyao
- Kwetu sisi wanawake wote: Tusikubali kununuliwa, kutishwa au kurubuniwa kwa njia yoyote. Kwa raia wote wa Tanzania, tutambue kwamba hatima ya Taifa letu iko mikononi mwetu na hivyo tusikubali kudanganywa na wagombea wachache wenye fedha kuuza kura zetu, kwani kufanya hivyo ni kuuza Utu wetu na Utu wa Taifa letu.

Madai kwa Serikali tutakayoipa dhamana ya kuliongoza Taifa letu kwa kupitia kura zetu:

Serikali itakayopata ushindi itambue kwamba kura za wanawake zimekuwa Turufu ya Ushindi kwao!!! Hivyo basi, punde itakapokuwa madarakani iwajibike kutimiza ahadi za kujenga Taifa la umoja wa kitaifa ikiwa ni taifa lililojengwa na wanawake kwa wanaume. Serikali tutakayoipa dhamana ya kutuongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, inawajibika kuweka mazingira wezeshi ya kujenga taifa linaloongozwa na demokrasia shirikishi na yenye kuheshimu haki za wanawake na makundi yaliyowekwa pembezoni. Ni jukumu la serikali tutakayoiweka madarakani kufanya mambo yafuatayo:

- Kuimarisha utekelezwaji wa misingi ya usawa kama ilivyobainishwa kwenye Katiba yetu ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania, na kwenye mikataba ya kimataifa na kikanda kuhusu haki za wanawake na makundi yaliyoko pembezoni
- Kubainisha mikakati ya kuondoa ubaguzi wa jinsia kwenye nyanja zote kama ilivyobainishwa kwenye dira ya Taifa 2025(Vision 2025)
- Katika uteuzi wa viongozi kwenye ngazi zote kusipungue asilimia 30 ya kikatiba lakini lengo liwe kufikia asilimia 50 kama serikali yetu ilivyokubali katika itifaki ya Maputo na Tamko la AU pamoja na Tamko la SADC.

- Kuboresha mikakati iliyoko na kubuni mikakati mipya ya kupunguza pengo la jinsia katika siasa, uchumi na ustawi wa jamii
- Kuzingatia misingi ya utawala bora, uwazi, na ushirikishaji katika kutekeleza mipango yote ya kuliendeleza Taifa letu
- Kuja na mikakati madhubuti itakayoanisha jinsi gani serikali inatambua mchango wa wastaafu/wazee waliokua katika sekta zisizo rasmi, hususani, sekta ya kilimo ambapo, asilimia kubwa ni wanawake.
- Kukemea vitendo vyote vyenye kudhalilisha Utu wa mwanamke pamoja na kuchukua hatua stahiki kwenye kutambua na kuenzi michango ya wanawake katika shughuli za kuliendeleza taifa letu.
- Kuimarisha jitihada za kukuza uchumi wenye kujikita kwenye msingi wa usawa na haki za wanawake
- Kuhakikisha kwamba vipaumbele vya Taifa vinaendana na mahitaji na vijaumbele vya wanawake katika kujikomboa kiuchumi, kisiasa, na katika ustawi wa jamii.
- Uhai wa wanawake wakati wanapojifungua uwekwe kwenye mipango na vipaumbele vya taifa.

4. HITIMISHO

Sisi Wanawake wapiga kura, kwa sauti moja, tunatoa hii Ilani ikiwa ni jumuishi ya sauti zetu na madai yetu kwa wadau wote wa uchaguzi. Kwa sauti moja tunasema,

> **“HAKI YA KUSHIRIKI KWENYE MEZA YA MAAMUZI NI HAKI YETU SISI SOTE NA TUNAIDAI.”**

MAPENDEKEZO

MAPENDEKEZO

S.L.P 8921, Mabibo
Dar es salaam - Tanzania
Simu: +255 754 784 050
Barua pepe: info@tgnp.org
Tovuti: www.tgnp.org
@tgnpmtandao